# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
# OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO,

## MHESHIMIWA DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM),

## AKIWASILISHA MWELEKEO WA UCHUMI MWAKA 2022 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022/2023

**Juni, 2022**

## YALIYOMO

**YALIYOMO** ........................................ i

**UTANGULIZI** ........................................ 1

**MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA 2021/2022** ........................................ 5

Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2021 ........................................ 5

Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar ........................................ 9

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI 2022** ........................................ 14

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ILIYOPATA FEDHA ZA SHIRIKA LA KIFEDHA DUNIANI (IMF) ZA KUHUISHA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI 2022** ........................................ 19

**MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022 NA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022/23** ........................................ 22

Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia. ........................................ 22

Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar ........................................ 22

**MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023** ........................................ 25

**RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023** ........................................ 32

Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji ........................................ 33

**MAENEO MTAMBUKA** ........................................ 35

Maandalizi ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 ........................................ 35

Mazingira ........................................ 36

Masuala ya Watu Wenye Ulemavu....................................................38

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya........................................38

Maambukizi ya UKIMWI ..................................................................39

Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto .......................................39

**MAJUMUISHO ..........................................................................40**

**HITIMISHO ................................................................................41**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika Baraza hili baada ya majadiliano ya bajeti za mafungu mbalimbali kwa Wizara na Taasisi za Serikali. Mkutano huu wa saba (7) wa Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni muhimu katika kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

2. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2021 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 pamoja na Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar 2022 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2021 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Mwaka 2021/22 kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022. Vile vile, nawasilisha vitabu vya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023.

3. **Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii imezingatia Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa 2021-2026 (Zanzibar Development Plan-ZADEP), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) ya 2030, Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC-Vision 2050) Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063 (African Development Agenda 2063). Mpango huu umezingatia Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Baraza

la Kumi (10) la Wawakilishi na ahadi anazozitoa anapokutana na wananchi katika nyakati tofauti. Hotuba hii ndiyo msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 nitakayowasilisha katika Baraza hili Tukufu leo alaasiri.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tunashuhudia namna anavyoendelea kuiongoza Zanzibar kwa amani, mshikamano, busara, hekima na umahiri mkubwa na kuendeleza mashirikiano na nchi pamoja na Mashirika ya Kimataifa mbalimbali. Aidha, niungane na Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani na wananchi wenzangu kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ujasiri na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi wake kikamilifu. Jitihada na uoni wake wa kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kijamii katika kuinua hali za wananchi zinaonekana wazi katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.

5. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kuwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla wakiwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais kwa uongozi wao mahiri, usimamizi, uchapakazi na uzalendo kwa nchi yetu. Juhudi zao zinaendelea kuleta mafanikio katika sekta zote nchini. Vile vile, nachukuwa fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kusimamia vyema Utumishi wa Umma ambao ndio msingi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuongoza Kamati ya Makatibu Wakuu ambao ndio masuuli wa fedha za umma. Tunawaombea wote kwa Mwenyezi Mungu awape afya njema waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi (Amin).

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa, naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wasaidizi wake wakuu Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulitumikia Taifa letu. Juhudi za viongozi hawa za kuiletea Tanzania Maendeleo zinaonekana wazi wazi katika kuitangaza, kutafuta fedha kupitia kwa Washirika wa Maendeleo na kushajihisha uzalishaji wa ndani kwa kuvutia wawekezaji. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape wepesi viongozi wetu katika kusimamia na kuendelea kutekeleza majukumu yao ipasavyo (Amin).

7. **Mheshimiwa Spika,** kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Wazanzibari wote kuwa nitatekeleza jukumu hili kwa bidii, weledi, uadilifu na uzalendo wa kiwango cha hali ya juu. Namshukuru Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais-Ikulu ambae alikuwa mtangulizi wangu katika Afisi hii kwa misingi mizuri ya kazi aliyoiweka ambayo imewezesha tufanye kazi zetu kwa ufanisi zaidi. Pongezi ziende vile vile kwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango; Mheshimiwa Ali Suleiman Mrembo kwa kuendelea kusimamia pia majukumu ya Ofisi yetu.

8. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Mwaka 2022/2023 zimezingatia dhana ya ushirikishwaji wa wadau katika hatua za uandaaji na maamuzi katika ngazi zote Serikalini. Ni vigumu kuwataja wadau wote waliotoa maoni na ushauri hadi kufikia hapa, lakini ni vyema nitambue mchango mkubwa wa Baraza lako Tukufu chini ya uongozi wako Spika

Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ukisaidiwa na Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma pamoja na Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma. Usimamizi wenu unaleta tija katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kufikia malengo tuliyojipangia ambayo yanatokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050. Mipango hiyo ni nguzo muhimu kwangu na kwa Baraza letu hili. Tunatoa pongezi zetu za dhati kwa Mheshimiwa Abdulla Hussein Kombo kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kumsaidia majukumu Mheshimiwa Spika. Tunaamini kuwa utendaji na usimamizi wake wa kazi utaleta matokeo mazuri. Kwa upande wetu, tunaahidi kumpa mashirikiano yetu katika kufikia matarajio ya Baraza, Serikali na Zanzibar kwa ujumla.

9. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani (CCM) na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri makini waliotupatia. Maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti na katika vikao mbalimbali vya mashauriano kwa kipindi cha mwezi Januari na Machi 2022 yamezingatiwa katika uandaaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23. Uandaaji wa hotuba hii umepata kwa kiasi kikubwa michango, ushauri na busara za Kamati hiyo. Kwa heshima ya pekee, nawapongeza waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwatumikia vyema wananchi majimboni mwenu. Nasi hatuna budi kulipa fadhila tulizopewa na wananchi kwa kuwaletea maendeleo.

10. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukrani naomba kuwasilisha kwa muhtasari wa Mapitio ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2021 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2022 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA 2021/2022

11. Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2021 ni kwa mujibu wa mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla (Macroeconomic indicators) ikiwemo Pato la Taifa, Kasi ya Mfumko wa Bei, Hali ya Ukosefu wa Ajira na Biashara ya Nje ikilinganishwa na mwaka 2020 na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2021-Machi 2022) kwa mujibu wa hali halisi ya kifedha.

### Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2021

*Uchumi wa Dunia*

12. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Shirika la Fedha la Dunia (IMF) ya mwezi wa April 2021 inaonesha kuwa, mwaka 2021, Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imefikia wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia -3.1 mwaka 2020. Hii inatokana na kurejea kwa shughuli za kiuchumi kwa kuendelea kusambazwa na matumizi ya chanjo ya UVIKO-19 na hatua za kuinua chumi za nchi mbali mbali. Ukuaji wa uchumi kwa makundi tofauti ya Nchi ilikuwa ni kama ifuatavyo:-

    i. Ukuaji wa uchumi kwa Nchi Zilizoendelea umefikia wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia -4.5 kwa mwaka 2020. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa uzalishaji wa malighafi pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa rasilimali watu;

    ii. Ukuaji wa Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi umefikia wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2021, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia -2.0 mwaka 2020. Kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za rejareja pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa miradi ya wananchi kwa nchi hizi ndio kumepelekea ukuaji huo;

iii. Kwa Nchi za Afrika kasi ya ukuaji imefikia wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia -2.1 mwaka 2020. Ukuaji huu umetokana na kuimarika kwa uchumi wa nchi nyingi za Afrika ambazo zinategemea sana utalii;

iv. Kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya ukuaji uchumi kwa mwaka 2021 imekua na kufikia wastani wa asilimia 4.5 kutoka wastani wa asilimia -1.7. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa uzalishaji kwenye kilimo na kuongezeka kwa bei za bidhaa zinazo safirishwa nje;

v. Kasi ya ukuaji wa Nchi za Afrika Mashariki imefikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2020. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kwa nchi hizi.

**Mwenendo wa Mfumko wa Bei Duniani**

**13. Mheshimiwa Spika,** kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta ya Nishati, Madini na huduma kwa mwaka 2021 kumesababisha kuongezeka kwa kasi ya mfumko wa bei kufikia wastani wa asilimia 4.4 kutoka wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2020. Hata hivyo, kasi ya mfumko wa bei una sura tofauti kwa mujibu wa maeneo yake kijiografia kama ifuatavyo:-

i. Kasi ya mfumko wa bei kwa Nchi Zilizoendelea imefikia asilimia 2.8 mwaka 2021 kutoka asilimia 0.7 mwaka 2020. Hii imechangiwa na kupanda kwa bei za nishati ya mafuta na vyakula pamoja na kuongezeka kwa gharama za Usafirishaji;

ii. Kasi ya mfumko wa bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi imepanda na kufikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2020. Kutokana na kuongezeka kwa bei za chakula na kuongezeka kwa bei za bidhaa za viwandani pamoja na kuongezeka kwa gharama za pembejeo;

iii. Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka kufikia wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2020. Hii ni kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta, ambayo imesababisha kuongezeka kwa mfumko wa bei wa nishati ya mafuta;

iv. Hata hivyo, kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2020. Hii ni kutokana na kuimarika kwa usambazaji wa chakula katika masoko ya ndani ya nchi na kwa nchi wanachama na kuwepo kwa utulivu wa bei za bidhaa kwa nchi hizi pamoja na sera bora za kifedha.

14. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na machafuko ya kisiasa yanayoendelea kwa nchi za Ulaya Mashariki tunashuhudia kupanda kwa bei za bidhaa muhimu duniani. Machafuko hayo yameathiri uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa hizo duniani ikiwemo mafuta, gesi, sukari na unga wa ngano. Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022 hali ya mfumko wa bei kwa bidhaa katika soko la dunia umekuwa kama ifuatavyo: Bei ya nishati za mafuta ilifikia wastani wa Dola za Kimarekani 96.3 kwa pipa ikilinganishwa na Dola 59.3 mwaka 2021. Bei ya unga wa ngano ilipanda na kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 432.6 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 275.2 kwa tani mwaka 2021. Bei ya sukari imeongezeka na kufikia wastani wa Dola 410 za Kimarekani kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 350 kwa tani mwaka 2021.

*Biashara ya Nje*

15. **Mheshimiwa Spika,** Biashara ni kichocheo kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuongezeka upatikanaji wa fedha za kigeni, kutoa fursa za ajira na kuongeza mapato ya Serikali nchini. Zanzibar ni miongoni mwa nchi za visiwa yenye fursa nzuri ya ushindani wa kibiashara katika upande wa usafirishaji na uagiziaji

wa bidhaa na kwa kipindi kirefu imekuwa kitovu cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki. Mwaka 2021, usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 155.6 bilioni kutoka thamani ya TZS 65.6 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 137.1. Kuongezeka thamani ya usafirishaji imechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji na usafirishaji wa zao la karafuu na mwani mwaka 2021.

16. **Mheshimiwa Spika**, Usafirishaji wa zao la karafuu kwenda nje ya nchi kwa mwaka 2021, umeongezeka na kufikia jumla ya tani 6,775.5 zenye thamani ya TZS 115.3 bilioni ikilinganishwa na tani 3,506.8 zenye thamani ya TZS 38.3 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2020. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa mavuno ya zao la karafuu kutokana na msimu mkubwa wa zao hilo. Kwa upande wa zao la mwani, usafirishaji umeongezeka na kufikia tani 12,611.1 zenye thamani ya TZS 11.9 bilioni mwaka 2021 ikilinganishwa na tani 11,382.6 zenye thamani ya TZS 11.7 bilioni mwaka 2020 zilizosafirishwa nje ya nchi mwaka 2020, ambayo ni sawa na ongezeko la thamani ya asilimia 2.2. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hili na kuongezeka kwa bei ya mwani katika soko la dunia.

***Hali ya Ukosefu wa Ajira***

17. **Mheshimiwa Spika,**Kwa mujibu wa utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanyakazi uliofanyika mwaka 2020/2021, Zanzibar ina kiwango cha watu walio katika uwezo wa kufanya kazi (labour force employment ratio) cha asilimia 76. Kati yao 61.1 wapo katika ajira kutoka Serikalini, Mashirika, Taasisi na Makampuni binafsi. Aidha kiwango cha ukosefu wa ajira kimeongezeka kutoka asilimia 17.4 mwaka 2014/2015 hadi kufikia asilimia 19.7 mwaka 2020/2021. Kwa upande wa vijana wenye uwezo wa kufanyakazi kati ya miaka 15 hadi 35, kiwango cha ukosefu wa ajira kimeongezeka zaidi kutoka asilimia 24.6 mwaka 2014/2015 hadi kufikia asilimia 27.6 mwaka 2020/2021. Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazoendelea (developing country) hivyo

kipato cha nchi hakiwezi kutosheleza kuwaajiri vijana wote. Hata hivyo, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021-2026, makadirio ya Kiwango cha ukosefu wa ajira ni kupungua na kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2026. Miradi mipya na inayoendelea inategemewa kwa kiasi kikubwa kupunguza viwango vya ukosefu wa ajira.

**Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar**

18. **Mheshimiwa Spika,** Juhudi za kuimarisha uchumi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zimeleta mafanikio katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya kiuchumi. Pato halisi la Taifa (GDP at Constant Prices) kwa mwaka 2021 lilifikia thamani ya TZS 3.275 trilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 3.116 trilioni mwaka 2020 sawa na kasi ya ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.1 kwa mwaka 2021. Ongezeko hilo ni kubwa ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 1.3 kwa mwaka 2020 kulikosababishwa na athari za UVIKO-19 kwa kuyumba sekta ya utalii na mdororo wa uchumi kwa nchi washirika wetu wa kibiashara. Aidha, Pato la Taifa kwa Bei ya Soko (GDP at Current Price) limeongezeka kufikia thamani ya TZS 4.633 trilioni mwaka 2021 kutoka thamani ya TZS 4.209 trilioni mwaka 2020.

19. **Mheshimiwa Spika,** Kufikia mwaka 2021, Zanzibar inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao 1,713,000. Hivyo, Wastani wa Pato kwa Mtu lilikadiriwa kufikia TZS 2,704,000 sawa na Dola za Kimarekani 1,171 ikilinganishwa na TZS 2,526,000 sawa na Dola za Kimarekani 1,099 mwaka 2020 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 7.0.

20. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu za ukuaji wa Uchumi kwa mwaka 2021 ni pamoja na:-

    i. Kuongezeka kwa Uingiaji Watalii nchini kwa asilimia 51.2 kufikia watalii 394,185 mwaka 2021 kutoka watalii 260,644 mwaka 2020;

ii. Kuongezeka kwa usafirishaji wa Zao la Karafuu kufika tani 6,775.5 zenye thamani ya TZS 115.3 bilioni mwaka 2021 kutoka tani 3,506.8 zenye thamani ya TZS 38.3 bilioni;
iii. Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji ambapo kwa mwaka 2021 jumla ya miradi 97 yenye thamani ya TZS 2.6 trilioni iliwekezwa ikilinganishwa na miradi 34 yenye thamani ya TZS 513.3 bilioni mwaka 2020;
iv. Kupatikana kwa ajira 7,791 kwa mwaka 2021 kutoka ajira 1,256 mwaka 2020 zilizotokana na miradi ya uwekezaji iliyoidhinishwa;
v. Kuongezeka kwa Usafirishaji wa zao la Mwani kufikia tani 12,611.1 zenye thamani ya TZS 11.9 bilioni mwaka 2021 na kutoka tani 11,382.6 zenye thamani ya TZS 11.7 bilioni mwaka 2020.

*Mwenendo wa Bei*

21. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2021, mfumko wa bei ulikuwa tulivu kutokana na Serikali kutoa punguzo maalum la ushuru kwa bidhaa za vyakula zikiwemo sukari, mchele na unga wa ngano pamoja na kutoa na kusimamia bei elekezi kwa bidhaa mbali mbali zilizoingia nchini ikiwemo bidhaa ya saruji na nondo. Hali hii ilipelekea upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini na bidhaa zote muhimu. Utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani kwa pamoja vilifanya mfumko wa bei kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo ulipungua kutoka wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2020 hadi asilimia 1.7 mwaka 2021. Mfumko wa bei za bidhaa za chakula ulipungua kufikia wastani wa asilimia 0.6 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2020. Kwa upande wa bidhaa zisizo za chakula kasi ya mfumko wa bei ulipanda kidogo kufikia wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2020.

22. **Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, kasi ya mfumko wa bei katika kipindi cha Januari hadi Machi 2022 inaonesha kuwa umepanda kufikia wastani wa asilimia 3.0 kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa za nishati ya mafuta, unga wa ngano na sukari katika soko la dunia. Serikali imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ikiwemo kutoa punguzo la ushuru na kusamehe baadhi ya tozo zinazokusanywa na Serikali ili wananchi wasipate athari ya ongezeko la mfumko wa bei nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Machi kwa nchi za Afrika Mashariki mfumko wa bei umefikia tarakimu mbili kinyume na kigezo cha chini ya asilimia tano (5) kilichowekwa na Jumuia ya Afrika Mashariki: Kenya asilimia 17.1, Tanzania asilimia 11.1, Uganda 11.8, Rwanda asilimia 20.3 na Burundi asilimia 42.1.

**Mwenendo wa Sarafu Thamani ya Shilingi**

23. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa tulivu ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,310 kwa mwaka 2021, ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,298 kwa mwaka 2020 sawa na kupungua thamani kwa asilimia 0.5. Hata hivyo, kasi ndogo ya kupungua kwa thamani ya shilingi ya Tanzania imetokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania katika usimamizi wa Sera za Fedha na Bajeti, kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nje ya nchi pamoja na kusimamia misingi ya uwazi katika ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni nchini.

***Sekta ya Utalii***

24. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii ni sekta kiongozi (leading sector) katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Kwa mujibu wa Utafiti wa Uingiaji wa watalii (Tourism Satellite Account 2019), utalii unachangia zaidi ya asilimia 29.2 katika Pato la Taifa. Serikali imeendelea kutangaza vivutio vipya vya utalii ndani na nje ya nchi na kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya kitalii

kwa kushirikiana na wananchi na sekta binafsi. Katika mwaka 2021 idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 51.2 kufikia watalii 394,185 kutoka watalii 260,644 mwaka 2020. Nchi ambazo ziliongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2021 ni Urusi asilimia 17.8 ikifuatiwa na Ufaransa asilimia 9.5, Poland asilimia 9.4, Afrika ya Kusini asilimia 5.1, Ujerumani asilimia 4.2, Ukraine asilimia 3.7, Uingereza asilimia 2.9 na Ubelgiji asilimia 2.9. Kwa wastani, nchi 23 zilizobakia zilichangia asilimia 45 ya watalii walioingia nchini.

*Sekta ya fedha*

25. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya fedha ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi. Sekta hii kwa mwaka 2021 imeweza kuchangia kwa asilimia 3.5 katika Pato la Taifa. Sekta ya fedha inajumuisha huduma za Mabenki, Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Soko la Mitaji na Dhamana, na Mifumo ya malipo na huduma ndogo ndogo za fedha (Microfinance) na imekua kwa wastani wa asilimia 9.9 mwaka 2021.

*Sekta ya Nje*

26. **Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa Zanzibar tunaingiza bidhaa nyingi muhimu kutoka nje ya Zanzibar (Net importers). Kwa mwaka 2021 nakisi ya biashara imeongezeka na kufikia thamani ya TZS 812.9 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 781.8 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 3.9.

27. **Mheshimiwa Spika** Thamani ya Usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka kutoka TZS 65.6 bilioni mwaka 2020 na kufikia TZS 155.7 bilioni mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 136.8 Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la Karafuu kufika tani 6,775.5 zenye thamani ya TZS 115.3 bilioni mwaka 2021 kutoka tani 3,506.8 zenye thamani ya TZS 38.3 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 93.2. Kwa upande wa usafirishaji wa zao la Mwani umefikia tani 12,611.1 zenye thamani ya TZS 11.9 bilioni mwaka 2021 kutoka tani 11,382.6 zenye

thamani ya TZS 11.7 bilioni mwaka 2020. Thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeongezeka na kufikia TZS 968.6 bilioni mwaka 2021 ikilinganishwa na thamani ya TZS 847.4 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Uagiziaji huo unahusisha bidhaa za vyakula, mafuta, vipuri , mashine na vifaa vya ujenzi.

**Mwenendo wa Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Intra trade).**

28. **Mheshimiwa Spika,** tunaelewa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya mahitaji ya chakula yanapatikana kutoka nje ya Zanzibar ikiwemo Tanzania Bara. Katika kipindi chote cha mwaka 2021 uhaulishaji wa bidhaa uliimarika na kupelekea upatikanaji wa mahitaji ya bidhaa zote za lazima. Uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 33.9 bilioni kutoka thamani ya TZS 15.0 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 126.1. Kwa upande mwengine kwa mwaka 2021 uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 288.2 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 243.8 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 18.2.

***Ukuzaji Rasilimali***

29. **Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa hali ya uwekezaji imeimarika kwa mwaka 2021. Kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) jumla ya miradi 97 yenye thamani ya mtaji wa TZS 2.6 trilioni iliidhinishwa ikilinganishwa na miradi 34 yenye thamani ya mtaji TZS 513.3 bilioni mwaka 2020. Kati ya miradi hiyo, miradi 28 yenye thamani ya TZS 200.5 bilioni sawa na asilimia 29 ya miradi inamilikiwa na wazawa na miradi 69 yenye thamani ya TZS 2.4 trilioni sawa na asilimia 71 ya miradi inamilikiwa na wageni. Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji kumepelekea kupatikana jumla ya ajira 7,791 mwaka 2021 ikilinganishwa na idadi ya ajira 1,256 zilizoripotiwa mwaka

2020 sawa na ongezeko la ajira 6,535: Kati ya ajira hizo miradi ya uzalishaji viwandani imechangia jumla ya ajira mpya 2,779 sawa na ongezeko la ajira kwa asilimia 35.6 mwaka 2021, miradi ya hoteli na migahawa imechangia jumla ya ajira mpya 2,043 sawa na ongezeko la ajira kwa asilimia 26.2, miradi ya afya na kazi za kijamii zimechangia jumla ya ajira mpya 900 sawa na ongezeko la asilimia 11.5 na shughuli za ujenzi zimechangia jumla ya ajira mpya 520 sawa na ongezeko la asilimia 6.6 mwaka 2021 na miradi ilobakia imechangia kwa asilimia 21.1.

## *MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI 2022*

30. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/22 ulikuwa ni mwanzo wa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) (2021-2026). Mpango wenye kauli mbiu inayosema Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu (Blue Economy for Inclusive Growth and Sustainable Development). Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022 ulilenga kutekeleza jumla ya Programu 25 na Miradi 39 na kupangiwa jumla ya TZS 882.8 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 606.5 bilioni sawa na asilimia 69 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka katika vyanzo vya ndani na TZS 276.3 bilioni sawa na asilimia 31 zilipangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 72.3 bilioni ni misaada na TZS 204 bilioni ni mikopo. Aidha, kati ya fedha hizo TZS 288.7 bilioni zilipangwa kugharamia Programu na Miradi ya Vipaumbele, TZS 204.4 bilioni kutoka Serikalini na TZS 84.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

31. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2021-Machi 2022, jumla ya TZS 212.5 bilioni sawa na asilimia 24 ya TZS 882.8 bilioni zilitumika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 91.8 bilioni sawa na asilimia 15 ya lengo la TZS 606.5 bilioni zilitoka Serikalini na TZS 121.1

bilioni sawa na asilimia 44 ya lengo la TZS 276.3 bilioni zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha jumla ya TZS 3.2 bilioni zimetumika kutekeleza kazi za kawaida ambazo ni Kuimarisha Usimamizi wa kukabiliana na Maafa, Uhuishaji na Ustahimilivu wa Utalii Zanzibar, Kuimarisha Uongozi wa Ushiriki wa Vijana katika Stadi za Maisha, Afya ya Uzazi na Mtoto, Uzalishaji wa Takwimu za idadi ya watu, Afya ya Mazingira na Hifadhi ya Mtoto kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

32. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo unafanyika kwa ufanisi, miradi mbali mbali ilipewa kipaumbele kufikia malengo ya maendeleo na kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi. Utekelezaji wa Programu na miradi kumi na tatu (13) ilipewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022. Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022, miradi sits (6) ya vipaumbele kati ya kumi na tatu (13) sawa na asilimia 46.1 iliingiziwa fedha. Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele kwa Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha ustawi wa uchumi na maisha ya watu ni kama ifuatavyo:-

i. **Programu ya Umwagiliaji Maji:** Programu hii ilianza mwaka 2018 na ilitegemewa kukamilika mwezi wa June, 2022 ikiwa na lengo la kuongeza uzalishaji wa mpunga na kupunguza uagiziaji wa bidhaa hii kutoka nje. Hadi kukamilika kwake, imepangiwa kutumia jumla ya TZS 115 bilioni. Kwa mwaka wa fedha, 2021/22 Programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 25.8 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 2.9 bilioni kutoka Serikalini na TZS 22.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 jumla ya TZS 16.1 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 63. Kati ya fedha hizo, TZS 1.9 bilioni sawa na asilimia 67 kutoka Serikalini na TZS 14.2 bilioni sawa na asilimia 62 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Programmu hii imefikia asilimia 90 ya utekelezaji. Kazi inayoendelea ni kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, uwekaji wa nguzo za umeme katika

bonde la Cheju A, uwekaji sawa wa Bonde la Mlemele pamoja na umaliziaji wa ujenzi wa mitaro na barabara za mashambani (farm roads).

ii. **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Elimu:** Programu ilianza mwaka 2017/18 na inategemewa kukamilika 2024/25 ikiwa na lengo la kuimarisha sekta ya elimu kwa ujenzi na kuweka miundombinu muhimu. Hadi kukamilika kwake, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 270 bilioni. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 57.0 bilioni ambapo TZS 34.2 bilioni sawa na asilimia 60 kutoka Serikalini na TZS 22.8 bilioni sawa na asilimia 40 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Katika kipindi cha miezi tisa (9) kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022, Programu hii imeingiziwa jumla ya TZS 5.5 bilioni kati ya fedha hizo TZS 3.2 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 9 na TZS 2.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 10 ya fedha zilizopangwa ambazo zimetumika kwa kazi za ukarabati wa Skuli ya Paje Mtule na Chwaka Tumbe, kazi ya usafishaji wa tarazo na utiaji wa waya za madirisha unaendelea pamoja na uwekaji nyaya za umeme kwenye maabara za skuli hizo zimefanyika.Utekelezaji wa Programu umefikia asilimia 87.

iii. **Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi–Mangapwani:** Katika kukuza uchumi wa Zanzibar, Serikali imeona kuna haja ya kuwa na bandari za kisasa jumuishi katika eneo la Mangapwani zitakazosaidia usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 mradi huu umepangiwa TZS 3.0 bilioni Hadi kufikia Machi, 2022, mradi huu umeingiziwa TZS 708 milioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 24 ya fedha zilizopangwa. Kazi zilizopangwa ni matayarisho ya awali ya eneo ikiwemo uwekaji wa miundombinu ya lazima ikiwemo maji na umeme, kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi (Master plan) katika eneo hilo na ulipaji wa fidia. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022, Kazi iliyofanyika ni uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ambao tayari umekamilika kwa hatua za kutafuta wawekezaji.

iv. **Mradi wa Uendelezaji wa Visima vya Ras El Khaimah:** Mradi huu ulianza mwaka 2013 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2022. Jumla ya visima 150 vimechimbwa Unguja na Pemba kwa awamu tatu tofauti. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Ras el Khaimah na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama Zanzibar hasa katika maeneo ya vijijini. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya TZS 8.0 bilioni zilipangwa kutumika kutoka serikalini. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 1.6 bilioni sawa na asilimia 20 ya fedha zimepatikana. Kazi zilizofanyika ni ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 0.4 kutoka kwenye kisima hadi tangi la maji katika eneo la Kitogani imekamilika na wananchi wananufaika na huduma hiyo. Aidha, ujenzi wa vichwa vya visima (well head block) na ununuzi wa pampu upo katika hatua za manunuzi. Ulipaji wa fidia kwa waathirika wa mradi wapatao 69 wameshalipwa katika maeneo ya Upenja (1), Kibweni (29), Kandwi (12), Mkokotoni Kicheche (22) na Mangapwani (5).

v **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Awamu ya Pili (Phase II):**Programu hii ilianza mwaka 2021/22 na inategemewa kukamilika 2024/25. Programu hii inagharamia ujenzi wa Ofisi za Serikali katika maeneo ambayo yamependekezwa kutoka Serikalini kwa lengo la kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili kutoa huduma nzuri na stahiki kwa wananchi. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya TZS 76.4 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 34 bilioni sawa na asilimia 45 zimepatikana kutoka Serikalini. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kufanya shughuli zifuatazo:

- ✓ Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na Vya Kati (SMIDA). Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuongeza thamani ya bidhaa na ubora wa vifungashio ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Ni ujenzi wa jengo lenye ghorofa moja (1) ambao umeanzia mwezi Agosti 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Juni 2022.

Jumla ya TZS 3.2 bilioni zilipangwa kugharamia mradi huo hadi kukamilika kwake. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 676 milioni sawa na asilimia 21 zimepatikana ambapo ujenzi umefikia asilimia 60 ya utekelezaji. Kazi zilizofanyika ni kukamilisha ujenzi katika ghorofa ya kwanza pamoja na ujenzi wa kibanda cha walinzi, ukuta na njia kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum (ramp). Aidha, kazi zinazoendelea ni usukaji wa nondo kwa ajili ya kupiga zege ya ghorofa ya pili, upigaji plasta, uchimbaji wa mashimo ya vyoo, uwekaji wa waya za umeme, uwekaji miundombinu ya TEHAMA na kamera za usalama (CCTV).

- ✓ Ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu: Jengo hilo la Mahkama Kuu limejengwa kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi na wananchi wanaofuata huduma. Mradi huu umeanza mwaka 2019, ulipangiwa jumla ya TZS 16.8 bilioni hadi kukamilika kwake, na ulipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Kwa mwaka wa fedha, 2021/2022 umeingiziwa jumla ya TZS 2.3 bilioni kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa ujenzi. Ujenzi huu umekamilika na jengo limeanza kutumika kwa shughuli za kimahakama.

- ✓ Aidha, jumla ya TZS 31.0 bilioni zilizobakia zimehaulishwa katika mafungu mbalimbali ya kibajeti kuruhusu matumizi ya fedha za kuhuwisha uchumi za mkopo nafuu wa Shirika la Fedha la Dunia (IMF).

vi. **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z Boost Inclusive Growth Zanzibar)** Programu ina lengo la kuimarisha hali ya maisha na kukuza Maendeleo ya kiuchumi katika maeneo yaliyoteuliwa ya Zanzibar katika utoaji wa huduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji. Programu hii ni mwendelezo wa programu ya kwanza ya Zanzibar Urban Services Project (ZUSP) ambayo ilimalizika muda wake mwezi Disemba 2020. Programu imepanga kutengeneza miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha maisha ya wenyeji katika

maeneo ya aina tatu ya Zanzibar: a) Mjini (b) Maeneo ya mjini yanayokuwa kwa haraka na (c) Mijini na vijiji vinavyoanzishwa na maendeleo jumuishi ya eneo maalum. Kwa mwaka 2021/22 programu hii imepangiwa jumla ya TZS 5.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kwa kipindi cha miezi 9 Julai 2021 hadi Machi 2022, imeingiziwa TZS 8.7 bilioni sawa na asilimia 152. Programu imetumia jumla ya TZS 118 milioni sawa na asilimia 2 na kutekeleza shughuli za uratibu na uendeshaji wa programu.

33. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa miradi mengine ya maendeleo iliyotekelezwa kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022 unaonekana katika Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2021 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/22.

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI ILIYOPATA FEDHA ZA SHIRIKA LA KIFEDHA DUNIANI (IMF) ZA KUHUISHA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI 2022

34. **Mheshimiwa Spika,** Serikali katika kukabiliana na athari za Ugonjwa wa Korona (UVIKO 19) imepokea jumla ya TZS 230.0 bilioni ikiwa ni asilimia 17.8 ya mkopo wote uliotolewa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Shirika la Fedha Duniani ndani ya mwaka wa fedha 2021/22. Mkazo uliwekwa kusaidia sekta zilizopata athari zaidi za Uviko 19. Hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeelekeza pesa hizo kwenye programu ya kuhuisha uchumi na kuendeleza jamii ili kurejesha hali za wananchi kwa kuendeleza shughuli zenye kuleta matokeo ya haraka na tija zaidi kwa wananchi wa maeneo mbali mbali. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imezielekeza fedha hizo katika kutekeleza miradi katika sekta za Elimu, Afya, Maji, Nishati na Uwezeshaji (Uchumi wa Buluu, Kilimo, Tawala za Mikoa, Vijana na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya). Fedha ziligaiwa kwa sekta zifuatazo: Sekta ya afya ilipangiwa TZS 78.5 bilioni; Sekta ya elimu TZS 68.5 bilioni; Sekta ya uwezeshaji wananchi kiuchumi TZS

35.5 bilioni; Sekta ya Maji TZS 34.2 bilioni; Sekta ya Nishati TZS 11.5 bilioni na TZS 1.8 bilioni kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya miradi.

35. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Afya imepangiwa jumla ya TZS 78.5 bilioni kwa kutekeleza miradi ya Ujenzi wa hospitali kumi (10) za Wilaya kwa Unguja na Pemba na hospitali moja (1) ya Mkoa wa Mjini Magharibi, hadi kufikia Machi 2022 jumla ya TZS 19.2 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 24.4. Kwa ujumla Ujenzi umefikia katika hatua mbali mbali na fedha zinatolewa kwa mujibu wa mikataba ambayo ina makubaliano baina ya mkandarasi na Serikali. Kwa Sekta ya elimu jumla ya 68.5 bilioni zimepangwa na hadi kufikia Machi jumla ya TZS 17.5 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 25.5 zimetolewa na kutekeleza shughuli za Ujenzi wa Skuli nane (8) za ghorofa na mbili (2) za mjumuisho katika maeneo ya Mtopepo, Mwanakwerekwe, Kwabinti Hamran, Kidogo chekundu na Jendele kwa upande wa Unguja na Makangale, Mwambe, Kwale na Pujini kwa upande wa Pemba unaendelea na uko katika hatua nzuri. Aidha Ujenzi wa madarasa ya mfano unafanyika katika maeneo ya Mbuyumaji madarasa manne (Kaskazini Unguja), Unguja Ukuu madarasa matano (Kusini Unguja), Kihinani madarasa manne (Mjini Magharibi), Maziwani madarasa saba (Kaskazini Pemba) na Ng'ombeni madarasa manne (Kusini Pemba).

36. **Mheshimiwa Spika,** Katika Sekta ya Uwezeshaji wananchi jumla ya TZS 35.5 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 30 bilioni zimetolewa sawa na asilimia 84.5 kwa ununuzi wa boti 577 za uvuvi ambapo kampuni sita za (Amos Industries Limited, Songoro Marine Transport Ltd, Captain Andy's Supply, Ocean Enterprises Limited, Dhow Licius na DMG) tayari zimeshafunga mikataba na zipo katika hatua mbali mbali za utengenezaji. Aidha utengenezaji wa boti 500 kwa ajili ya ubebaji wa mwani unaendelea kupitia Quiro Company Limited na Fibre Dynamics.

37. **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya maji ilipangiwa jumla ya TZS 34.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 9.2 bilioni sawa na asilimia 27 zimepatikana na kuanza ujenzi wa vibanda vinane (8) kwa ajili ya kuhifadhia mashine na mitambo ya kusukumia maji kwa upande wa Unguja na uko katika hatua ya linta. Vibanda hivyo viko katika maeneo ya Shakani kwa Mussa Elimu, Kisakasaka Miembeni, Fuoni Sai, Fuoni Jangamizini, Chumbuni, Mbuzini kwa Sheha, Selem na Fuoni Jitimai.

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika sekta ya nishati jumla ya TZS 11.5 bilioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2022, jumla ya TZS 11.5 bilioni sawa na asilimia 100 zimetolewa na kufunga mikataba saba (7) kwa wazabuni wa ununuzi wa vifaa vya umeme ikiwemo nguzo, waya na mita. Jumla ya nguzo 480 kutoka kwa mzabuni Poles Ltd zimeshapokelewa na ZECO.

39. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya TZS 1.8 bilioni zimepangwa kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, magari, usimamizi na ufuatiliaji. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 935 milioni zimetumika kama ifuatavyo: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali TZS 200 milioni, Tume ya Mipango TZS 296 milioni, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) TZS 100 milioni, Mkaguzi wa Ndani wa hesabu za Serikali TZS 75 milioni na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya TZS 264 milioni.

40. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya vijana 13,870 walipata ajira za muda katika taasisi mbali mbali ambazo zinatekeleza miradi hio. Katika ajira hizo ni kama ifuatavyo: sekta ya elimu imeajiri vijana 7,119, sekta ya afya imeajiri vijana 2,331, sekta ya uwezeshaji wananchi kiuchumi imeajiri vijana 4,266 na sekta ya maji imeajiri vijana 154.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022 NA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022/23

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022

### Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia.

41. **Mheshimiwa Spika,** Wakati mgogoro wa Ukraine na Urusi ukiendelea, athari zake na hasa kiuchumi zinaendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali ulimwenguni ikiwemo barani Afrika. Mataifa mbali mbali duniani yameshatahadharisha kwamba vita hivyo vinavyoendelea vitasababisha ongezeko la bei za bidhaa na kuzorotesha shughuli za maendeleo.

42. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) makadirio ya ukuaji wa uchumi ni kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2022 kinyume na matarajio ya awali ya ukuaji wa asilimia 4.4 kutoka asilimia 6.1 kasi ya ukuaji wa mwaka 2021.

*Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar*

43. **Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2022 ni kwa mujibu wa viashiria vya uchumi jumuishi na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar kwa Mwaka 2022/2023. Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023 umeandaliwa kwa kuzingatia misingi ya mipango ya awali iliyolenga kuimarisha na kukuza uchumi jumuishi wenye kuhimili ushindani. Katika kutekeleza Mpango wa mwaka 2022/2023, msukumo mkubwa umewekwa katika kuiwezesha Zanzibar kutumia kikamilifu fursa zilizopo ili kujenga uchumi wenye ushindani, kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, kuendeleza sekta ya viwanda kwa maendeleo ya wananchi wote.

*Malengo na Shabaha za Uchumi Jumuishi kwa Mwaka 2022/2023*

44. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, shabaha za uchumi jumuishi zilizozingatiwa katika Mpango ni kama ifuatavyo:-

    (i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2022;

    (ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja;

    (iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 24.7 ya Pato la Taifa mwaka 2022/2023 kutoka wastani wa asilimia 19.6 ya mwaka 2021/2022;

    (iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 18.1 ya Pato la Taifa mwaka 2022/2023 kutoka asilimia 15.8 mwaka 2021/2022; na

    (v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

45. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya ukuaji wa uchumi ilitarajiwa kufikia wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022 kutokana na sababu zifuatazo:-

    i. Kupatikana kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na mkopo maalum kutoka Benki Kuu ya Tanzania;

    ii. Kuendelea kuongezeka kwa uingiaji wa watalii na kukadiriwa kufikia watalii 450,213 kwa mwaka 2022 ikiwa hali ya dunia itaendelea kuwa salama bila ya migogoro. Matarajio ya kuongezeka kwa watalii hapa Zanzibar, yanachangiwa na dalili zilizoanza kuonekana mara baada ya Uzinduzi wa Filamu ya Tanzania, ***The Royal Tour*** ambayo imeshirikisha viongozi wetu wakuu wa nchi ambao ni Mheshimiwa Samia

Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

iii. Matarajio ya kuongezeka kwa mapato ya ndani kwa asilimia saba (7%) kutokana na utekelezaji wa mikakati inayofanywa na Serikali ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielekroniki kwa ukusanyaji wa mapato na kuondoa misamaha ya kodi isiyo na tija;

iv. Kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji viwandani, ikiwemo uwekezaji mkubwa kwenye visiwa vidogo vidogo, uzalishaji wa nguo kutoka kiwanda cha Basra, kiwanda cha maji Chamanangwe na kiwanda cha viatu cha Amani. Matarajio ya uwekezaji pia katika maeneo mengine mengi, ikiwemo uwekaji wa mawe ya msingi, ufunguzi na kuanza kazi kwa Hoteli za Kitalii za madaraja mbali mbali zikiwemo Hoteli ya Marijani, Riu, Palolo na L'oasis ambazo zitasaidia katika kutoa huduma za kitalii na kuzalisha ajira hapa nchini.

v. Kuimarika kwa shughuli za kibiashara hasa kwa wajasiriamali wadogo wadogo baada ya kupatikana kwa fedha za mkopo nafuu;

vi. Kudhibiti kwa matumizi ya Serikali kupitia kuimarika kwa mifumo ya mapato na matumizi ya kibajeti ikiwemo mfumo wa BAMAS na kuelekeza matumizi hayo katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

vii. Kuimarika kwa huduma za abiria na mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amaan Karume ambako kutawezesha kuhudumia ndege za kubwa za kimaitafa zinazofika Zanzibar kwa viwango cha kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, kutokana na kuibuka kwa vita vya Urusi na Ukraine hivi karibuni kumepelekea athari kubwa za kiuchumi duniani kote. Kwa upande wa Zanzibar athari zinazotarajiwa kujitokeza ni pamoja na:-

i. Kupungua kwa sekta ndogo za Uzalishaji na Usafirishaji wa Bidhaa kutokana na kupanda kwa bei za nishati ya mafuta;

ii. Ongezeko la bei za bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula;

iii. Matumizi makubwa ya fedha za kigeni za kuagiza bidhaa nje ya nchi ikiwemo nishati ya mafuta, hali hii inaathiri akiba ya fedha za kigeni ya nchi na kupunguza matumizi ya fedha hizo;

iv. Hofu ya kupungua kwa Watalii kutoka nchi za Urusi na Ukraine ambapo kwa miaka ya karibuni watalii kutoka nchi hizo waliongezeka. Kwa mwaka 2021 walifikia 85,196 sawa na asilimia 21.5.

46. **Mheshimiwa Spika,** Kufuatia hali hii, Zanzibar inatarajiwa kuendelea kuathirika kiuchumi na matarajio mapya ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2022 ni kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 5.4 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2021.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

47. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Mwaka 2022/2023 ni muendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 wenye kaulimbiu ya "Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu".

48. **Mheshimiwa Spika,** Mpango huu utatekeleza miradi na programu ambazo utekelezaji wake una azma ya kufikia malengo yaliyowekwa na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050. Hivyo, miradi ya kimkakati kwa mwaka 2022/2023 inaakisi maeneo matano (5) yaliyotajwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano. Maeneo hayo ya kimkakati ni: Kutumia fursa za uchumi wa buluu; Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu; Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; Kuimarisha Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; Utawala Bora na Uhimili.

### a) Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

49. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha uchumi wa buluu, Serikali inatarajia kutumia TZS 30 bilioni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari za uvuvi za kisasa katika maeneo ya Shumba Mjini kwa upande wa Pemba na Kizimkazi kwa Unguja. Kuendelea na taratibu za ununuzi wa meli za uvuvi na matayarisho ya mitambo ya kukaushia mazao ya baharini jumla ya TZS 13.8 bilioni zitatumika. Aidha, kwa kushirikiana na Sekta binafsi, Serikali inatarajia kuanzisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza maboti na kusarifu samaki na dagaa na vyumba vya baridi (cold storage). Jumla ya TZS 11.0 bilioni zimetengwa ikiwa ni mchango wa Serikali katika miradi hiyo. Vile vile, Serikali itaendelea na ujenzi wa kiwanda cha mwani pamoja na mabwawa ya uzalishaji na ufugaji wa majongoo bahari na kuazishwa kwa mashamba ya mwani. Katika kutumia fursa za Uchumi wa Bluu, Serikali pia, inaendelea na mpango maalumu wa kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia uwekezaji katika uvuvi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba na nyenzo zikiwemo boti za uvuvi na ukulima wa mwani. Serikali pia itaanza ununuzi na uandaaji wa mifumo ya uhifadhi na usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia.

### b) Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu

50. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, Serikali imepanga kuendelea na kuanza ujenzi wa barabara mbali mbali Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 505.2 ikiwemo barabara ya Mkoani – Chake Chake km 43.5, Fumba – Kisauni km 12, barabara ya Tunguu – Makunduchi km 48, Barabara ya Chake Chake – Wete km 22.1, Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 pamoja na Barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa Kilomita 103.7. Jumla ya TZS 415.3 bilioni zinatarajiwa kutumika katika kazi hizo.

51. **Mheshimiwa Spika,** Tunaelewa kuwa kwa miaka mingi tumekuwa na changamoto ya usafirishaji wa mizigo kutokana na kuwa na

miundombinu hafifu na chakavu ya bandari zetu. Maandalizi ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani (Intergrated Port) itakayojumuisha bandari za Mizigo, uvuvi, chelezo, mafuta na gesi yameanza kwa kutafuta wawekezaji kuja kuwekeza katika Bandari hiyo katika maeneo tofauti yaliyoainishwa katika Mpango Mkuu (Master Plan) wa ujenzi wa bandari hiyo yanaendelea. Wawekezaji wengi wamejitokeza kwa ajili ya kushiriki katika kupata fursa ya uwekezaji na kwa sasa Serikali ipo katika hatua ya kutathimini na kuwapata wawekezaji wenye sifa na uwezo wa kuwekeza katika bandari hizo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya upelekaji wa miundombinu ni TZS 8.0 bilioni.

52. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa ardhi ya Zanzibar inapangwa na kutumika kwa uangalifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi, Serikali iko katika hatua za kutayarisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi ( National Land Use Plan). Pia itaendelea kupanga ardhi katika sehemu za makaazi, maeneo ya viwanda na uwekezaji, maeneo ya hifadhi pamoja na maeneo ya bahari. Serikali imekusudia kutumia mifumo ya kidijitali katika kufanya kazi ya kupima na kuyapanga maeneo ambayo bado hayajapimwa na kupangwa. Taasisi zinazosimamia masuala ya ardhi, itahakikisha maeneo hayo yatagawiwa kwa wananchi na wawekezaji wenye kuhitaji kwa kuzingatia haki pamoja na usawa. Maeneo ya Kibele, Shakani na Ndijani Mseweni kwa Unguja na Mfikiwa, Finya na Pagali kwa Pemba yatapimwa na kugawiwa kwa wananchi wenye mahitaji bila ya upendeleo au ubinafsi wa aina yoyote.

53. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya TZS 134.1 bilioni zitatumika kuanza kwa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba na kwa malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa kiwanja hicho. Kati ya fedha hizo, Serikali itatoa TZS 8.0 bilioni kwa kuwalipa fidia wananchi na kiasi cha TZS 126.1 bilioni zitakua ni mkopo nafuu ambazo Zanzibar itachukua kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

54. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya nishati itaimarishwa kwa upatikanaji wa nishati mbadala ya umeme kutokana na nguvu za jua kupitia mradi wa Mageuzi wa Sekta ya Nishati (Zanzibar Energy Sector Transformation and Accessibility-ZESTA). Serikali inatarajia kulipa fidia jumla ya TZS 6.5 bilioni zitatumika kuwalipa wananchi watakaoathirika wakati wa ujenzi wa njia za kusafirishia umeme na maeneo ya uzalishaji umeme na TZS 11.3 bilioni ni kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi ikiwa ni fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Aidha, Serikali pia itaendelea kuhimiza wawekezaji binafsi kuingia katika uzalishaji wa nishati ya umeme ili kuweza kukidhi mahitaji kutokana na mageuzi makubwa ya kiuchumi ambayo yatahitaji mahitaji makubwa ya umeme.Ili kukabiliana na mahitaji ya Umeme yanayojitokeza kutokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali na Sekta Binafsi unaoendelea, Serikali ina mpango wa kuifanyia ukarabati wa mkonga wa umeme " submarine cable" ya zamani ya 40 megawati pamoja na kufanya mazungumzo na wawekezaji binafsi kuja kuwekeza katika uzalishaji wa umeme utakaokuwa na bei nafuu zaidi.

### c) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

55. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kuweka miundombinu imara kwa ajili ya kukuza biashara ya Kitaifa na Kimataifa hapa Zanzibar kwa kuanza ujenzi wa vituo vya biashara na maonesho. Kwa mwaka 2022/2023 Serikali imepanga kutumia TZS 4.0 bilioni kwa ajili ya kupeleka miundombinu ya maji, umeme na barabara katika eneo la Nyamazi. Serikali inatarajia kukuza biashara ya ndani na kuvutia wafanyabiashara wa kimataifa mara baada ya eneo hili ambalo litakuwa na miundombinu yote inayohitaji kukamilika. Maeneo mengine ambayo yamepangwa katika kusaidia mageuzi ya kiuchumi ni pamoja na ujenzi wa "Industrial Parks" kwenye maeneo ya Dunga, Pangatupu, Micheweni na Chamanagwe. Matayarisho ya awali ya kuandaa upembuzi yakinifu kwa kushirikiana na Afroexim yameanza. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na kampuni binafsi itajenga Kituo cha Mikutano

cha Kimataifa kwa njia ya mashirikiano na Sekta Binafsi yaani EPC+Finance. Kituo hicho kitasaidia Zanzibar kukuza utalii wa mikutano hapa Zanzibar.

**d) Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii**

56. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itawapanga watumishi hao katika madaraja yao na kuwapatia mishahara kutokana na sifa zao ikiwemo elimu, uzoefu pamoja kada maalumu zinazohitajika. Serikali pia itaendelea kujenga uwezo wa watumishi pamoja na kuwapatia mafunzo kwa lengo la kuongeza ujuzi wao, ndani na nje ya nchi.

57. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) Nambari 2 ya mwaka 2005 kila mwajiri anapaswa kuwasilisha asilimia 15 ya michango ya wafanyakazi wake kwa utaratibu maalum kama ulivyoelezwa kisheria na kupokea mafao baada ya kutimiza umri wa kustaafu wa miaka 60. Serikali kwa sasa inaifanyia mapitio Sheria hiyo ili kuimarisha hali za wafanyakazi ikiwemo kupewa mafao yao mara pale wanapopoteza ajira kwa sababu mbali mbali kama ilivyotokea kupotea kwa ajira nyingi wakati wa mripuko wa ugonjwa wa Uviko -19. Marekebisho ya Sheria hiyo yamezingatia kuwepo kwa fao jipya la upotevu wa ajira ambalo litawasaidia waajiriwa kurejesha ustawi wa maisha yao wakati wanapopoteza ajira katika umri wowote.

58. **Mheshimiwa Spika,** Katika uimarishaji wa huduma za kijamii Serikali inakusudia kuimarisha Sekta ya Elimu, Afya pamoja na Michezo. Katika sekta ya elimu, Serikali imepanga kuimarisha na kujenga Vituo vya Amali kwa kila Wilaya kwa ajili ya kuwapa vijana taaluma za vitendo ili waweze kujiajiri. Jumla ya TZS 33.2 bilioni zitatumika kwa ajili ya shughuli hizo ambapo TZS 28.7 bilioni zitatolewa na Washirika wa Maendeleo na TZS 4.5 bilioni zitatolewa na Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023. Serikali pia, itaendelea kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili iweze

kukidhi mahitaji ya wanafunzi wanaoomba mikopo kwa ajili ya kukidhi ufadhili wa programu mbali mbali. Serikali pia, itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kimataifa na nchi nyenginezo, kutafuta na kupata nafasi za masomo kwa njia ya ufadhili wa programu mbali mbali.

59. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imepanga kununua vifaa tiba na vya maabara za uchunguzi kutokana na ujenzi unaoendelea wa hospitali za Wilaya na Hospitali ya Mkoa Unguja na Pemba pamoja na uimarishaji wa hospitali zilizopo na zinazoendelea kujengwa.

60. **Mheshimiwa Spika,** Kwenye mkakati wa kuimarisha sekta ya michezo, Serikali imepanga pamoja na mambo mengine, kuimarisha na kujenga viwanja vya michezo kwa kila Wilaya ili kukuza sekta ya michezo kwa vijana. Kwa mwaka 2022/2023 ujenzi utaendelea katika viwanja vikiwemo Kitogani Unguja na Kishindeni, na Kangani kwa Pemba. Jumla ya TZS 4.0 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

### e) Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili

61. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuimarisha utawala bora na uhimili, Serikali inatarajia kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za kesi (Electronic Case Management Information System - ECMIS). Jumla ya TZS 1.0 bilioni zimetengwa kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo huo ambao utasaidia uharakishaji wa uendeshaji wa kesi pamoja na kuweka uwazi katika uendeshaji wa kesi. Vile vile, jumla ya TZS 5.6 bilioni zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Mahkama za Mikoa na kwa kuanzia Mahkama ya Mkoa wa Kusini Pemba.

62. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha mazingira ya kazi yanaimarika kwa watumishi wa umma ili waweze kutoa huduma bora zaidi na endelevu kwa wananchi, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa mji wa Serikali utakaojumuisha ofisi za mawizara na taasisi mbali mbali. Jumla ya TZS 92.2 bilioni zitatumika katika ujenzi wa mji huo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023. Ofisi nyingi za Serikali zitajengwa katika eneo moja ili kurahisisha upatikanaji

wa huduma. Kwa sasa maeneo kadhaa yametembelewa yakiwemo Dunga,Tunguu na Kisakasaka kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ili kuweza kupata eneo stahiki ambalo litakidhi mahitaji ya ujenzi wa ofisi hizo. Vile vile, Serikali itaendelea kufanya ukarabati wa majengo, ujenzi ofisi mpya, kuweka mifumo ya kidijitali ya utendaji kazi na kuwapatia stahiki wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria na Taratibu.

63. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kusimamia utoaji wa huduma bila ya ubaguzi wa rangi, jinsia, eneo mtu analotoka, imani yake ya dini au siasa. Katika kuimarisha msingi wa amani na utulivu nchini ambao ni muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali itaendelea kuimarisha Taasisi na mifumo yake ili kudhibiti vitendo vyovyote vitakavyoashiria uvunjifu wa amani na kusababisha kutetereka kwa umoja wa kitaifa uliopo Zanzibar.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla utekelezaji wa maeneo ya kimkakati yatagharimu TZS 762.0 bilioni katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

65. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inatarajia kutekeleza miradi mengineyo muhimu ambayo itagharimu TZS 590.1 bilioni katika mwaka wa fedha wa 2022/2023. Sehemu kubwa ya fedha hizi, zitatumika kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi inayoendelea, malipo ya fidia na upelekaji wa miundombinu katika maeneo yanayotarajiwa kutekelezwa. Miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika Kitabu cha Pili.

66. **Mheshimiwa Spika,** Maeneo mengineyo ambayo Serikali itaangalia ni pamoja na kuhakikisha ushirikishwaji wa sekta Binafsi, taasisi za kifedha, wafanyabiashara, Washirika wa Maendeleo na jumuiya zisizo za kiserikali na wananchi kwa ujumla katika kutekeleza miradi itakayoleta maendeleo ya haraka na yenye tija ikiwemo miradi ya mashirikiano ya sekta

ya umma na sekta Binafsi (PPP) na uwekezaji Binafsi. Katika kuimarisha dhana ya mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi kazi za ujenzi wa masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi, Chuini – Kwanyanya zinaendelea pamoja na kuanza kwa ujenzi wa soko la Machomanne, ukarabati wa soko Kongwe la Darajani, Ukamilishaji wa ujenzi wa maduka Darajani pamoja na ujenzi wa kituo cha kisasa cha kuegesha magari. Aidha, Serikali ilishajiisha kuwekeza kwa pamoja katika maeneo mbali mbali yakiwemo ujenzi wa vituo vya usarifu na uhifadhi wa bidhaa za samaki na mazao mengine ya baharini; ujenzi wa dakhalia za vyuo vikuu, ujenzi wa kituo cha maonesho ya bishara na mikutano, uwekaji wa nishati ya jua katika visima vya maji na ujenzi wa vituo vikuu vya mabasi ya abiria Kariakoo kwa Unguja na Chanjaani kwa Pemba.

67. **Mheshimiwa Spika,** Sekta Binafsi ina mchango mkubwa katika Kukuza uchumi wa maendeleo ya jamii. Kwa kuzingatia hilo Serikali inashajiisha uwekezaji kwenye maeneo mbali mbali ikiwemo:- (i) Ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya baharini na kusarifu matunda; (ii) Kuanzisha mashamba ya kufugia samaki na Majongoo ya bahari; (iii) Ujenzi wa hospitali ya Rufaa na kufundishia – Binguni; (iv) Ujenzi wa viwanda vya dawa; (v) Ujenzi wa nyumba za makaazi za bei nafuu; na (vi) Ujenzi wa viwanja vya michezo na burudani.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 1,352.19 bilioni zinakadiriwa kutumika ili kugharamia Mpango wa Maendeleo katika mwaka wa fecha wa 2022/2023. Kati ya fedha hizo, TZS 682.54 bilioni ni kutokana na mapato ya ndani, TZS 669.65 ni mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara, misaada na mikopo nafuu kutoka nje.

69. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa kufanya yafuatayo: Kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kupanuka kwa wigo wa kodi; kuimarisha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari ikiwemo kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA na kutoa elimu kwa umma; kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi; kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kuoanisha na kuboresha tozo na ada. Vile vile, Serikali itaimarisha usimamizi wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa uratibu wa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi ya maendeleo (D-fund Management Information System) pamoja na kuimarisha maandalizi ya mapema ya miradi ya maendeleo.

**Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji**

70. **Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ni moja ya nyenzo muhimu inayowezesha utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Tume ya Mipango itaendelea kutumia mbinu na viashiria vilivyoainishwa katika Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ili kupima utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 na kuchukua hatua za kutatua changamoto zitakazobainika katika utekelezaji. Aidha, miongozo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini ya Mpango ikiwemo Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 itaendelea kuzingatiwa. Tume ya Mipango imeanzisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kuongoza uratibu wa ufuatiliaji na tathmini ili kupata matokeo tarajiwa. Mfumo huo wa ufuatiliaji na tathmini umekamilika na mafunzo yametolewa kwa wahusika wote Serikalini na utaanza kutumika kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa mfumo huu, Tume ya Mipango itashirikiana na Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi katika kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango. Tume ya Mipango itapokea na kuchambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini kupitia Mfumo huu wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo – Monitoring and Evaluation System for Zanzibar Development Plan 2021-2026 kutoka kwa Taasisi zinazotekeleza miradi ya maendeleo. Vile vile, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango itaandaa na kutoa taarifa ya kila mwaka ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka na ule wa miaka mitano yaani ZADEP.

72. **Mheshimiwa Spika,** Serikali tayari imetoa maelekezo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafsiri malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 katika Mipango na Bajeti za kisekta kwa mwaka 2022/23 pamoja na kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo na kuwajengea uwezo watumishi wa umma katika maeneo ya ufuatiliaji na tathmini.

73. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali itaendelea kuandaa na kutoa miongozo juu ya ukusanyaji, uchambuzi na uchakataji wa takwimu za viashiria vinavyosaidia katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango. Takwimu hizo zitapaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi wakati wa kuandaa taarifa za kitakwimu za mwenendo na matokeo ya utekelezaji wa Mpango.

## MAENEO MTAMBUKA

### Maandalizi ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022

74. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mara nyengine Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko katika maandalizi ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetangaza kufanya Sensa ya Watu na Makaazi ifikapo tarehe 23 mwezi Agosti 2022. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), ipo kwenye maandalizi ya kufanya Sensa hiyo. Sensa ya Watu na Makaazi ni zoezi la kitaifa linalofanyika kila baada ya miaka 10 ambapo Sensa ya mwisho kufanyika nchini ni ile ya mwaka 2012. Hivyo, Sensa ya mwaka 2022 itakuwa ni sensa ya Sita kufanyika nchini baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Sensa nyingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

75. **Mheshimiwa Spika,** Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini na kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makaazi yao katika nchi kwa kipindi maalum. Kwa maana nyingine, sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makaazi. Takwimu hizi za msingi ndizo zinazowezesha kuainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

76. **Mheshimiwa Spika,** Umuhimu wa kipekee wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ni pamoja na:-

    1. Kuisadia Serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia

shughuli za utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050, mageuzi ya masuala ya huduma za kijamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa;

2. Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za Wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali;

3. Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote;
4. Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano Pato la mtu mmoja mmoja, Pato la Taifa, Ajira na ukosefu wa Ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi;
5. Taarifa itakayowezesha Serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira; na
6. Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia. Takwimu sahihi za Sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika Serikali za Mitaa.

77. **Mheshimiwa Spika,** Hivyo, tunaomba kila mwananchi kwa nafasi yake kushajihisha na kutoa ushirikiano wa dhati ili tuweze kufanikisha zoezi hili kwa ufanisi uliokusudiwa. Takwimu sahihi zitaiwezesha Serikali kutunga na kufuatilia utekelezaji wa Sera kwa mujibu wa viashiria vya takwimu zitakazopatikana. Naomba nami kuchukua fursa hii kuwashajiisha wananchi wenzangu kuwa Tujiandae Kuhesabiwa kwa ajili ya Maendeleo yetu.

**Mazingira**

78. **Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyoelewa kuwa utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu. Tumekuwa tukishuhudia mabadiliko ya tabianchi ambayo yanatokana na uharibifu wa

mazingira na kupotea kwa misitu na miti ya asili. Jitihada kubwa zimefanyika katika uhamasishaji na utunzaji wa mazingira, lakini imebainika kuwa miti mingi inatoweka kutokana na ukataji usiozingatia Sheria hususan miti ya thamani kwa ajili ya majengo, makaazi, matumizi ya nishati na madawa na kupelekea kutoweka kwa bioanuai na uoto wa asili. Hadi kufikia mwaka 2022, Zanzibar ina misitu 10 ya hifadhi yenye ukubwa wa hekta 37,107.38. Jumla ya Shehia 45 (27 Unguja na 18 Pemba) zimetekeleza upandaji miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 119,389, kupitia Mpango wa Misitu ya Hifadhi ya Jamii ulioanzishwa mwaka 2013. Ripoti ya Sensa ya Miti ya mwaka 2013 imebainisha kuwa wastani wa hekta 1,200 za misitu zinapotea kila mwaka sawa na asilimia 1.2. Kwa mwaka 2022/2023, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar katika uhifadhi wa mazingira umelenga kupanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 10,000. Serikali imepanga kutekeleza Programu ya Kuifanya Zanzibar kuwa ya Kijani (Green Legacy of Zanzibar) kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a) Kuimarisha vitalu vya uoteshaji miche kwa Unguja na Pemba;

b) Kuanzisha na kuendeleza bustani za mimea (Botanical Gardens) angalau moja kwa kila Wilaya Unguja na Pemba;

c) Kuimarisha mazingira kwa kupanda na kurejesha miti ya aina mbalimbali katika Wilaya zote 11 za Unguja na Pemba; na

d) Kuhamasisha jamii kuendelea kuhifadhi mazingira kwa kupanda na kutunza miti pamoja na kuenzi siku ya upandaji wa miti kitaifa.

79. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii za pwani ya Zanzibar ujenzi wa matuta ya kuzuia uingiaji wa maji chumvi katika mashamba unaendelea pamoja na kuendeleza maeneo yaliyoharibika kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo ni Bwefum na Kizimkazi kwa Unguja na Sipwese, Kojani, Msuka na Kisiwa

Panza kwa Pemba. Utafiti wa kina kuhusu maeneo yaliyoathirika na Mabadiliko ya tabianchi (Climate Vulnerability Assessment) utafanyika.

### Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

80. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha haki na fursa kwa Watu wenye ulemavu zinakuzwa, Sheria Nambari 9 ya mwaka 2006 ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) inafanyiwa mapitio kwa ajili ya kujumuishwa zaidi Watu Wenye Ulemavu katika nyanja zote. Matarajio ya Sheria Mpya ni kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kupata elimu zaidi, kuajiriwa na kujiajiri, kupata huduma za afya na kupata fursa nyengine nyingi za kujiwezesha kiuchumi. Kupitia mipango iliyowekwa, suala la ufikiaji huduma, fursa na haki za Watu wenye Ulemavu limetiliwa mkazo. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuwatambua na kuwasajili watu wenye ulemavu ili kuweza kuimarisha mipango ya kuwawezesha kuishi maisha yao na kupunguza utegemezi kadiri inavyowezekana kwa upande mmoja na kwa upande mwingine, kuhakikisha visaidizi vinapatikana na kugaiwa kupitia Serikali, Washirika wa Maendeleo na watu binafsi katika jamii. Kwa sasa, Watu Wenye Ulemavu wanaotambulika katika Daftari la Usajili wamefikia 5,420 kati ya 76,647 waliobainika katika Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2012. Natoa wito kwa watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika Zoezi la Sensa la Mwaka 2022 ili Serikali iweze kujua idadi kamili ya watu wenye ulemavu waliopo na hivyo kuweza kupanga mipango mizuri kwa ajili ya kupata mahitaji yao, haki pamoja na fursa nyenginezo.

### Matumizi na biashara ya dawa za kulevya

81. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na kudhibiti biashara, uingizaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini jambo ambalo linadhoofisha nguvukazi ya taifa hasa vijana. Operesheni za kukamata watuhumiwa wa dawa za kulevya zitaendelea kufanyika katika maeneo mbali mbali huku msisitizo ukiwekwa katika milango mikuu ya kuingizia dawa za kulevya. Aidha,

jitihada za kurekebisha tabia na hali za watumiaji wa dawa za kulevya zitaendelea kupitia nyumba za upataji nafuu na kituo cha Serikali kilichopo Kidimni, ambacho pia kimeweka miundombinu ya uwezeshaji vijana walioacha matumizi ya dawa kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo, ufugaji na ufundi.

**Maambukizi ya UKIMWI**

82. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwingine, kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI na hatimaye kufikia lengo la dunia la kuondoa UKIMWI katika orodha ya Magonjwa hatarishi, Serikali imo katika hatua za kuandaa Mkakati mpya wa Kitaifa wa Nne ambao utabainisha mbinu za kuyafikia zaidi makundi maalum na kuweka mkazo katika kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na maambukizi kwa vijana, huku msisitizo wa kuwatambua na kuwaingiza katika utaratibu wa matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI yakitiliwa mkazo. Kwa sasa, Zanzibar maambukizi ya ukimwi yapo chini ya asilimia moja.

**Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto**

83. **Mheshimiwa Spika,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameridhia kuwa kinara wa uwezeshaji Wanawake kiuchumi katika Jukwaa la Kizazi chenye usawa (Generation Equality Forum GEF ) ambalo lilifanyika nchini Paris Ufaransa Julai 2021. Mheshimiwa Rais alikubali kuwa kinara wa eneo nambari mbili (2) linalohusu haki na usawa wa kiuchumi (Economic Justice and Right) kati ya maeneo sita yaliyoainishwa katika Jukwaa hilo. Katika kutekeleza hayo Mheshimiwa Rais ameteua Kamati ya Ushauri ya Kitaifa katika hatua za Utekelezaji wa eneo hilo la Haki na Usawa wa Kiuchumi. Kamati hiyo ina Wajumbe 25 kati ya hao 19 ni kutoka Tanzania Bara na wajumbe sita (6) kutoka Zanzibar wakiwemo wa Serikali, Taasisi binafsi, vyuo vikuu, Taasisi za fedha. Mpaka sasa Kamati hiyo ya kitaifa ya Ushauri, Uratibu na Ufuatiliaji wa Ahadi za Nchi katika Jukwaa hilo la Kizazi chenye Usawa (GEF) kwa kushirikiana na Secretarieti

inakamilisha Programu ya Taifa ya Utekelezaji ya kuanzia 2021 -2026, ambayo itatekelezwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Programu hiyo itakapokamilika utaandaliwa mfumo shirikishi na jumuishi kwa kushirikisha sekta na wadau mbalimbali. Lengo la Programu hii ni uwezeshaji Wanawake kiuchumi ikiwa ni nyenzo muhimu ya kumnyanyua Mwanamke kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Mwanamke kupata Teknolojia rahisi na sahihi katika kufanya shughuli za kiuchumi, kutolewa mafunzo ya ujasiriamali na utoaji wa mitaji kwa wanawake pamoja na uwepo wa mifumo sahihi ya kidigitali katika shughuli za kiuchumi zinazofanywa na Wanawake. Kamati ya Kizazi chenye Usawa imefungua milango kwa makundi mengine kushiriki katika Usawa wa uwezeshaji wanawake kiuchumi.

**MAJUMUISHO**

84. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali, Mpango huu ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa kipindi cha Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye kaulimbiu ya "Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu". Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2022/23 unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa kuimarisha utulivu wa viashiria vya uchumi na kasi ya ukuaji wa uchumi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani hususan kwa kutumia mali ghafi za kilimo na uvuvi; kuongeza uwekezaji katika maeneo mbali mbali ikiwemo katika visiwa vidogo vidogo na katika maeneo huru ya kiuchumi; kuendeleza ujenzi wa miundombinu wezeshi na kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

85. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji kwa sekta binafsi na kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasilimali watu nchini hususan kwa kuwajengea uwezo vijana katika stadi za kazi za amali ili waweze kujiajiri na kuongeza tija katika uzalishaji; na kuchochea maendeleo ya watu kwa kuimarisha utoaji wa huduma muhimu zikiwemo za afya, elimu, maji na umeme kwa mustakabali wa maisha yao na kukuza uchumi wa Zanzibar.

## HITIMISHO

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru Washirika wote wa Maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Washirika wa Maendeleo wa Kimataifa na Wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ushirikiano wao umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ninawaomba waendelee kushirikiana na Serikali katika kutekeleza Mpango ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Naomba niwatambue washirika wa maendeleo na nchi rafiki zinazoendelea kushirikiana nasi kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na ACRA, AfDB, AMREF, BADEA, BASKET FUND, CHINA, CANADA, CIDA, CRDB, COSTECH, DANIDA, DFID, EAC, EDF, EU, EXIM BANK, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, HOPELAND UNIVERSITY, HIPZ, GN, GPE, GOOD NEIGHBOUR, IAEA, INDIA, IFAD, ILO, IMF, JAPAN, JICA, KHALIFA FUND, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOREA, KUWAIT, MALAYSIA, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - NETHERLAND, OMAN, OPEC, PBZ, PMI, QATAR CHARITY ORGANISATION, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, SWEDEN, THPS, TfT, UK, UN, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UNIDO, URT, USAID, UN WOMEN, UTURUKI, WORLD BANK, WHO na ZSSF.

87. **Mheshimiwa Spika,** Nitoe shukrani za dhati kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya hotuba hii. Aidha, ninawashukuru Makamishna wa Tume ya Mipango Nd. Ahmed Makame Haji –Kamishna wa Ukuzaji Uchumi; Nd. Siti Abbas Ali - Kamishna wa Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya kisekta na Kupunguza umaskini, Dkt.

Zuhura Mohamed Abdallah - Kamishna wa Ufuatiliaji na Tathmini, Dkt. Afua Khalfan Mohamed Kamishna wa Utafiti, Nd. Salama Ramadhan Makame - Kamishna wa Maendeleo ya Watendakazi; na watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh. Nawashukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Makatibu Wakuu Nd. Aboud Hassan Mwinyi na Nd. Rashid Said Rashid kwa kusimamia kikamilifu maandalizi ya taarifa hii.

88. **Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2021 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022 na Mwelekeo wa Hali ya uchumi wa Zanzibar 2022 na Mpango wa Maendeleo wa 2022/2023 vinapatikana katika tovuti ya Tume ya Mipango (http://planningznz.go.tz)

89. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23.

90. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MHESHIMIWA DKT. SAADA M. SALUM**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**
**ZANZIBAR**